JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI

715 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

Muda: Saa 3:30 **Jumatano, 16 Mei 2018 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na saba (17)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B na maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu C.
3. Sehemu A ina alama 40 na sehemu B na C zina alama 30 kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

1 814715 100011

DSEE-0518

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Ainisha mafunzo manne yatokanayo na historia ya nabii Adam (a.s).

2. Eleza kwa ufupi mambo manne juu ya wajibu wa mume kwa mkewe.

3. Katika uchumi wa Kiislamu, fafanua mambo manne ya kuzingatiwa katika ununuzi na uuzaji wa bidhaa.

4. Bainisha faida nne za kitabu cha kiada cha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa mwalimu na mwanafunzi.

5. Eleza kwa ufupi hoja mbili kuhusu mtazamo wa Qur'an juu ya ukewenza.

6. Bainisha vigezo vinne vinavyotegemewa katika uchaguzi wa njia na mbinu za kufundishia.

7. Bainisha hatua nne katika utengenezaji wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

8. Eleza kwa ufupi kuhusu mambo yafuatayo:
   (a) Umuhimu wa Zakatul-Fitri
   (b) Yanayopaswa kufanyiwa yatima.

9. Eleza kwa ufupi mambo manne muhimu ya kuzingatia utakapokuwa unatunga maswali ya mtihani wa Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa wanafunzi wako wa shule ya sekondari.

10. Wafuatao ni warithi wa marehemu Bi Zaynab:
    (a) Mume wake
    (b) Mtoto wake mmoja wa kiume
    (c) Mama yake mzazi na
    (d) Baba yake mzazi.

    Kwa kuzingatia maagizo katika Qur'an, ainisha fungu la kila mrithi wa Bi Zaynab.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **matatu** (3) kutoka sehemu hii.

11. Eleza kwa kina hasara nne zitakazopatikana kwa jamii inayofuata sera ya kudhibiti uzazi.

12. Onesha mambo manne yaliyowafanya muhadithina waiweke hadithi katika kundi la hadithi sahihi.

13. Jadili makosa manne miongoni mwa makosa ya "hudud" na jinsi ya kuyarekebisha katika mfumo wa sheria ya Kiislamu.

14. Fafanua vyanzo vinne vya mapato ya serikali ya kiislamu katika kipindi cha makhalifa wanne.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Thibitisha ukweli kuwa bila vifaa vya mtaala ni vigumu kufanikisha zoezi la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

16. Eleza mambo sita yanayoonesha umuhimu wa jedwali la kutahini kwa mwalimu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu anapoandaa mtihani.

17. Kwa kutumia hoja sita unga mkono kauli kuwa, "mtihani mzuri wa Elimu ya Dini ya Kiislamu ni ule uliochanganya maswali ya insha na ya majibu mafupi."

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner